**OFISINI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO**

**SHULE YA SEKONDARI NYANZWA**

**SLP 74**

**MAZOMBE -KILOLO**

**MZAZI/MLEZI WA**.......................................................

**YAH: MAWGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA 2021**

Nafurahi kukutaarifu ya kuwa mwanao amechaguliwa kunjiunga na shule hi KIDATO Cha kwanza 2021 kama mwanafunzi wa kutwa anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11/01/2021 SAA moja na nusu asubuhi akiambatana na MZAZI /MLEZI.

**SIKU YA KURIPOTI UJE NA VITU VIFUATAVYO:**

1) Nakala ya cheti Cha kuzaliwa

2) Begi la kubebea vitabu na Daftari

3) Taftari 9 kubwa (Countrer book), daftari ndogo 9, Mkebe na vifaa vyake.

4) Fomu ya daktari. Apimwe mtoto na TAARIFA zijazwe katika Fomu hiyo.

5) Fomu ya TAARIFA za mwanafunzi ijazwe kikamilifu.

6) Fomu ya kukubali nafasi hii ijazwe kikamilifu

**SHERIA ZA SHULE -** Sheria na kanuni za shule zinazingatia vipengere vifuatavyo.

A) Mwanafunzi anatakiwa kusimama wakati wote anakutana na mwalimu au mtu yeyote aliyemzidi umri.

B) Mwanafunzi hatakiwi kutumia lugha mbaya kwa WALIMU na kwa watu wengine.

C) Mwanafunzi aonyeshe umuhimu was kushirimi mazi za mikono kwa kujituma.

D) Mwanafunzi haruhusiwi kufanya Mambo yafuatayo:

i)Kutumia kilevi chochote

I)Kufuga kucha, nyele au ndevu.

iii) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima.

iv)Kugombana au kupigana.

v)Kujjhusisha na mapenzi(Uasherati)

vi)Kuhusika Katika wizi kwa namna yeyote ile.

vii) Mwanafunzi kuwa na simu kwa muda wote anapokuwa shuleni.

E) Mwanafunzi anatakiwa kukimbia mara moja kila anapoitwa.

**MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZKSHA MWANAFUNZI SHULE**

A) Kutumia kilevi

B) Wizi

C) Kujihusisha na mapenzi, kupata au kusababisha mimba

D) Kupigana, Kugombana au kusababisha vurugu.

E) Kutumia Lugha ya matusi

F) Utoro wa kudumu

**SARE ZA SHULE**

**A) WAVULANA**

1) Suruari rangi ya kijanijedhi yenye Malinda na mifuko miwili mbele mmoja nyuma.

2) shati jeupe mikono mifupi yenye kifuko upande wa kushoto.

3) Vatu vyeusi vya ngozi kwa kutunga na kamba vyenye kisigino kifupi na soksi nyeupe

4) Sweta rangi ya bendera ya Taifa

**B)WASICHANA**

1) Sketi rangi ya kijanijedhi (Mshono Linda box) Iwe ndefu kufunika soksi.

2) Blauzi jeupe mikono mifupi yenye kifuko upande wa kushoto.

3) Vatu vyeusi vya ngozi kwa kutunga na kamba vyenye kisigino kifupi na soksi nyeupe

4) Sweta rangi ya bendera ya Taifa

**TANBIHI:** kila Mwanafunzi aje na sare za michezo, bukta au traksuti rangi ya bluu.

Nakutakia maandalizi mema

Z.S. Fyataga
……………………….
MKUU WA SHULE
**NYANZWA SEKONDARI**